



The European Commission support for the production of this publication does not constitute an endorsement of the contents which reflects the views only of the authors, and the Commission cannot be held responsible for any use which may be made of the information contained therein.

WEKA VIWANJA VYA MICHEZO KATIKA HALI YA KIJANI

Country: Tanzania

Partner: TULOG



Asasi ya Tulime inatumia Klabu ya Mpira wa Miguu ya Udzungwa kuifikia jamii katika ya masuala ya ukusanyaji na uchakataji wa taka. Wachezaji wataungana na volunteers katika kutoa uhamasishaji kupitia mchezo wa mpira wa miguu, Mada hii itatatolewa kwa njia ya mkutano mfupi utakaofanyika kabla ya kuanza kwa mchezo wa mpira wa miguu na kutoa elimu kwa watu juu ya umuhimu wa usimamizi wa taka na Usafishaji; Wachezaji watahimizwa juu ya mambo makuu matatu katika kudhibiti taka amabyo ni Kutumia tena, Kukataa na Kuchakata. Washiriki wa mradi wa Youcom wataanda bango lenye ujumbe; “Weka viwanja vya michezo katika hali ya Kijani”.

Ukusanyaji wa takataka utafanywa katika viwanja vya michezo, wachezaji watashiriki katika kukusanya mifuko ya plastiki na chupa baada ya mechi, tayari kwa ajili ya uchakataji hii itakuwa kama sehemu ya kuboresha uwezo wa jamii kuchukua juhudi muhimu kwa ukusanyaji wa taka. Hii itasaidia kuhamasisha jamii kuishi na mazingira katika hali ya kirafiki na asili.



MPIRA WA MAKARATASI



Funded by the Erasmus+ Programme of the European Union

The European Commission support for the production of this publication does not constitute an endorsement of the contents which reflects the views only of the authors, and the Commission cannot be held responsible for any use which may be made of the information contained therein.



MCHEZO WA REDE

Timu itagawanywa katika makundi mawili kundi la kwanza litaunda vitu kwa kutumia chupa zilizokusanywa na kundi liingine litaunda vitu kwa kutumia mifuko ya plastiki. Vitu hivyo vitakavyoundwa vitajumuisha vitu kama mpira wa makaratasi au mifuko ya plastiki; Mpira huu hutumiwa na watoto wa kike kucheza mchezo wa rede na watoto wa kiume hutumia mpira huu kucheza mpira wa miguu hasa katika maeneo ya vijijini. Shughuli hii ya ubunifu itasaidia kuurudisha mchezo wa rede kwa watoto wa kike ambao unaonekana kupotea kadiri siku zinavyokwenda; pia itasaidia kuwahamasisha watoto kuwa mpira huu mhimu si tu kwa kuchezea bali unasaidia kutunza hali ya usafi katika mazingira wanamoishi kwani wameweza kutambua matumizi mengine ya mifuko ya plastiki.



KUTUMIA TENA CHUPA ZA PLASTIKI